# JARIDA MAALUM

*HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA*












## Maadhimisho ya siku ya Wanawake yalivyo fana Tandahimba

*Machi 8*
**2023**



# DED GAMA ATOA WITO KWA WANAWAKE KUPINGA UKATILI KATIKA JAMII

Kuelekea maadhimisho ya kilele cha siku ya Wanawake duniani Machi 8,2023 Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Ndg.Mussa Gama ametoa wito kwa wanawake kupinga vitendo vya ukatili katika jamii.
Ameyasema hayo Februari17,2023 wakati akizungumza na wanawake katika kijiji cha Malopokelo kilichopo kata ya Malopokelo ambapo amewasistiza kutoa taarifa ya vitendo vya kikatili katika vyombo husika.

# UWT TANDAHIMBA WAKABIDHI VIFAA HOSPITALI YA WILAYA

Kuelekea kilele cha maadhimisho ya siku ya wanawake duniani Machi 8,Umoja wa Wanawake wa CCM Wilaya ya Tandahimba wamekabidhi vifaa mbalimbali katika wodi ya wazazi,wodi ya watoto na wodi ya wanawake katika hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.
Vifaa hivyo wamekabidhi Februari 24,2023 ambapo pia walifanya usafi wa mazingira katika maeneo yanayozunguka majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Tandahimba







**Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe. Kanali Patrick Sawala akizungumza na wanawake wa Tandahimba.**

# KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI DC SAWALA ATOA WITO KWA WANAWAKE TANDAHIMBA

Kuelekea kilele cha maadhimisho ya siku ya wanawake duniani Machi 8,2023 Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe.Kanali Patrick Sawala ametoa wito kwa wanawake kuwa karibu na watoto ili kubaini changamoto zao sambamba na kupinga ukatili na unyanyasaji wa kijinsia katika jamii.
Amesema hayo Februari 24,2023,wakati akizungumza na wanawake wa Tandahimba waliojitokeza kwa wingi katika viwanja vya nje ya ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ambapo amesema kuwa wanawake wananyanyasika lakini wengine wanakaa kimya hawataki kusema.
"Wakina mama kuweni karibu na watoto ili kujua changamoto zao,ni wakati wa kusema unyanyasaji wa kijinsia na ukatili sasa basi,Serikali ipo nanyinyi,kuna madawati,msikae kimya,mnapoteza haki zenu kwasababu mnakaa kimya,lazima mseme ili vyombo husika vichukue hatua,"amesema Dc Sawala.
Aidha Dc Sawala alisikiliza kero mbalimbali za wanawake ambapo alizitolea ufafanuzi na zingine aliahidi kufuatilia kwa hatua zaidi,alitumia nafasi hiyo pia kuwapongeza wanawake wanavyoshiriki katika kuleta maendeleo sambamba na kushiriki katika matukio mbalimbali ya Kitaifa,Kimkoa na Kiwilaya ambapo amewasistiza kujitokeza kwa wingi kushiriki katika mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Aprili 5,2023 na kushiriki kilele cha siku ya wanawake ambapo Kimkoa maadhimisho hayo yatafanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba katika viwanja vya shule ya msingi Amani.
Naye Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Ndg. Mussa Gama Akizungumzia mikopo ya kuwawezesha wanawake kiuchumi ambapo Halmashauri inatoa asilimia 4 kwa wanawake amewasistiza kulipa kwa wakati ili wanawake wengine wenye uhitaji na wana sifa nao waweze kunufaika nayo.

# KATA 32 ZA HALMASHAURI YA TANDAHIMBA WAZINDUA MAJUKWAA YA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI

Kuelekea Maadhimisho ya kilele cha Siku ya Wanawake Duniani Machi 8,2023 Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba imezindua majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi kata zote 32 na vijiji vyake.
Uzinduzi wa majukukwaa hayo utasaidia wanawake kujikwamua kiuchumi katika maeneo yao sambamba na kutokomeza ukatili wa kijinsia na uchumi duni ili kujenga kizazi chenye usawa.
Aidha maadhimisho ya kilele cha siku ya wanawake Kimkoa yamefanyika Halmasahauri ya Wilaya ya Tandahimba katika viwanja vya shule ya msingi Amani ambapo Mgeni Rasmi ni Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe.Kanali Ahmed Abbas Ahmed.
Maadhimisho ya mwaka 2023 yameongozwa na kaulimbiu "Ubunifu na mabadiliko ya Teknolojia ,Chachu katika kuleta usawa wa Kijinsia"



**Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya yaTandahimba ndugu Mussa Gama akifafanua jambo kwa wanawake wa Tandahimba.**



**Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe. Kanali Patrick Sawala akiwa na wajumbe wa jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi wa Tandahimba.**

# DC SAWALA AZINDUA JUKWAA LA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA

Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe.Kanali Patrick Sawala amezindua Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ambapo amesistiza kutumia jukwaa hilo kujadiliana fursa na changamoto sambamba na kuweka mikakati ya kuweza kujitegemea kiuchumi.

Akizindua Jukwaa hilo leo Machi 2,2023 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri amesema kwamba jukwaa hilo litaondoa matabaka na kuweza kupata fursa ya kujua sheria ambayo itawasaidia kujua haki zao katika masuala mbalimbali.

Aidha ametoa rai kwa viongozi wa jukwaa hilo kusimamia miongozo,taratibu na sheria lengo wanawake waweze kujikomboa kiuchumi sambamba na kushirikiana na kuheshimiana ili kuweza kufikia malengo yao.

“ Nazindua rasmi Jukwaa hili la Wilaya,Jukwaa hili likawaunganishe,muhimu sana mpendane,mshirikiane na kuheshimiana ili kwa umoja wenu muweze kujikomboa kiuchumi na sambamba na hili nawaelekeza Halmashauri waweze kuandaa warsha na mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali ili kuwawezesha wanawake waweze kutumia fursa hizo kukuza uchumi ,” amesema Dc Sawala.



Naye Mratibu wa Dawati la Jinsia Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Bi.Neema Shungu amesema kuwa uundwaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi yameanzia ngazi ya kijiji,kata na Wilaya ambalo leo limezinduliwa rasmi.

Amesema kwamba uwezeshaji wa wanawake kiuchumi ni nguzo muhimu kwa kuhakikisha malengo ya maendeleo endelevu pamoja na malengo ya hamsini kwa hamsini ifikapo mwaka 2030 yanafikiwa.

# DC SAWALA AONGOZA MATEMBEZI YA HISANI TANDAHIMBA

Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe. Kanali Patrick Sawala ameongoza wananchi katika matembezi ya hisani ambayo yalianzia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuelekea soko la zamani na kuhitimisha viwanja vya shule ya msingi Amani sambamba na kufanya usafi wa mazingira.
Akihitimisha matembezi hayo katika viwanja vya shule ya msingi Amani Machi 4,2023 Dc Sawala alisema kuwa matembezi ya hisani yanalengo la kuamsha ari kwa wananchi kuelekea Siku ya Wanawake ambayo Kimkoa yamefanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.
Aidha amesema kwamba matembezi hayo pia yanalengo la kuamsha ari na kuleta ujumbe kwa wanatandahimba kushiriki katika uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Mkoani Mtwara Aprili 2,2023 na ujumbe wa kukaribisha na kuupokea Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Aprili 5,2023.
Pia Dc Sawala ametoa wito kwa wananchi kushiriki katika maandalizi ya Mwenge wa Uhuru ikiwa ni pamoja na kufanya usafi wa mazingira ili mwenge wetu uweze kupita na kuleta mshikamano.
Naye Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Ndg.Mussa Gama amesema kuwa kuelekea katika matukio hayo Halmashauri inaendelea na maandalizi mbalimbali.





## ASASI ZA KIRAIA TANDAHIMBA ZAKABIDHI VIFAA KWA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM

Kuelekea siku ya Wanawake Duniani Machi 8, 2023 Asasi za kiraia Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba zilikabidhi vifaa mbalimbali kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum waliopo katika shule ya msingi Mahuta bondeni kata ya Mahuta.
Vifaa hivyo wamekabidhi Machi 6,2023 shuleni hapo sambamba na kufanya usafi wa mazingira.
Asasi zilizoshiriki ni Shirika la Wanawake Wenye Uthubutu Tandahimba (WAO),TWAO,TABUFO na SDA ambapo wameahidi pia kuwakatia bima za afya ya ICHF wanafunzi 29 ili waweze kupata huduma za afya.
Maadhimisho ya kilele cha Siku ya Mwanamke Kimkoa yamefanyika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba katika viwanja vya shule ya msingi Amani.






# TACOBA WATOA ELIMU YA KIFEDHA KWA WAJASIRIAMALI WANAWAKE  TANDAHIMBA

Kuelekea Siku ya Mwanamke Duniani Benki ya Wananchi Tandahimba(TACOBA) ilitoa elimu ya kifedha kwa wanawake ili waweze kukuza  biashara zao sambamba na kukuza uchumi wao.
Akifungua mafunzo hayo Machi 6,2023 Meneja Mkuu wa TACOBA Wilaya ya Tandahimba Yahaya Kiyabo alisema kuwa mafunzo hayo ni kukumbushana ili wanawake waweze kufikia malengo yao ya kujikwamua kiuchumi sambamba na kutunza hesabu za kila siku za biashara zao.
Kwa upande wa Mratibu wa dawati wa jinsia Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Bi.Neema Shungu ametoa wito kwa wanawake wa vikundi waliohudhuria mafunzo hayo kuzingatia ili yaweze kuwasaidia katika shughuli zao za biashara za kila siku.

## Viongozi wa Wilaya washriki mradi wa amsha ari kata ya Lukokoda

Kuelekea siku ya Wanawake Duniani Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe.Kanali Patrick Sawala akiwa pamoja na KU,Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Ndg.Mussa Gama na Wakuu wa Idara na vitengo walishiriki kujaza kifusi katika mradi wa vyumba viwili vya madarasa Shule ya Sekondari Lukokoda.
Mradi huo umeibuliwa na wananchi wa Kata ya Lukokoda  ambapo shughuli ya ujazaji kifusi ilifanyika  Machi 7,2023 kwa kushirikiana na wananchi wa kata hiyo waliojitokeza kwa wingi.
Aidha Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilikabidhi saruji mifuko ishirini (20) kuunga juhudi za wananchi wa kata ya Lukokoda katika ujenzi mradi wa vyumba viwili vya madarasa.
Saruji hizo zilikabidhiwa mara baada ya shughuli ya kujaza kifusi kukamilika







**Mkuu wa mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed (katikati) akitoa neno, kulia ni Mbunge wa Tandahimba Mhe. Katani Katani, kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe. Kanali Patrick Sawala.**

# RC MTWARA ASEMA SERIKALI ITAENDELEA KUWAWEZESHA WANAWAKE KIUCHUMI

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe.Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema Serikali itaendelea kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kutambua na kuthamini mchango wao katika ukuaji wa Uchumi.

Amesema katika fedha zinazotolewa na Halmashauri kwa makundi maalum ya Vijana, Wanawake na watu wenye Ulemavu ambapo mwaka wa fedha 2021/2022 na Disemba 2022/2023 Halmashauri za Mkoa wa Mtwara kutokana na fedha za mapato ya ndani zimekopesha kiasi cha shilingi Bil 3.3 kwa vikundi 632 vikiwemo vya wanawake.

RC amesema katika fedha hizo shilingi Bil 1.7 zimetokana na makusanyo ya makundi husika,shilingi Bil 1.6 zimetokana na marejesho ,Shilingi Bil 1.6 zimekopeshwa kwa vikundi 356 vya wanawake na vijana,Shilingi Bil.1.3 vikundi 177 vya watu wenye ulemavu na shilingi Mil 345 kwa vikundi 145.

Aidha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri za Mkoa wa Mtwara zimeweka makadirio ya kukopesha kiasi cha shilingi Bil.2.4 kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu ambapo ametoa wito kurejesha mikopo hiyo kwa wakati sambamba na wanawake kuchangamkia fursa hiyo ili kujikwamua kiuchumi.

Amesema hayo Machi 8,2023 katika kilele cha maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani yenye kauli mbiu “Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia chachu katika kuleta Usawa wa Kijinsia” ambapo Kimkoa yamefanyika katika viwanja vya shule ya msingi Amani Halmasahauri ya Wilaya yaTandahimba na kutaka jamii kutathimini na kutafakari kwa pamoja jinsi Mkoa ulivyopiga hatua kutokomeza vitendo vya kikatili.

“Nachukua fursa hii kuhimiza wewe mjasiriamali kujenga hamasa binafsi ya kujifunza maarifa mapya yatakayokusaidia kuwa mbunifu katika biashara yako,nawapongeza wanawake wajasiriamali ambao mmejitokeza kuonesha bidhaa zenu ,taasisi zote na wananchi mlioshiriki katika siku hii ya wanawake ambayo imefana sana,”amesema RC.

Kwa upande wa viongozi mbalimbali waliopata nafasi ya kuzungumza wamesistiza wanawake kutokomeza vitendo vya ukatili kwa kutoa taarifa za ukatili unaofanyika katika jamii ili vyombo husika viweze kuchukua hatua za kisheria kwa wahusika.




Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Mhe.Baisa Baisa




Meneja wa Tanecu Tandahimba Bi.Sababu Juma akikabidhi Taulo za kike kwa Mkuu wa mkoa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed siku ya kilele cha siku ya Wanawake.




Afisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Mtwara Bi Tabitha Kilangi akisoma taarifa yake kwa Mgeni Rasmi.

# DC SAWALA ATEMBELEA MABANDA YA WANAWAKE WAJASIRIAMALI TANDAHIMBA

Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe.Kanali Patrick Sawala leo alitembelea mabanda katika maonesho ya wanawake wajasiriamali katika viwanja vya shule ya msingi Amani Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.
Maonesho hayo yalianza Machi 6,2023 ambapo wanawake wajasiriamali kutoka katika Halmashauri za Mkoa wa Mtwara walionesha bidhaa zao na kuuza kwa wananchi waliotembelea katika viwanja hivyo.



**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba**